TANGAZO LA SERIKALI NA. 625 la tarehe 1/9/2023

SHERIA YA UWAKALA WA MELI TANZANIA,
(SURA YA 415)

## AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 28 (3))*

AMRI YA NAULI ZA ABIRIA KATIKA NJIA YA MWANZA–BUKOBA KATIKA ZIWA VICTORIA YA MWAKA 2023

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Nauli za Abiria Katika Njia ya Mwanza–Bukoba Katika Ziwa Victoria ya Mwaka 2023.

Matumizi

2. Amri hii itatumiwa na Kampuni wakati ikitoa huduma katika njia ya Mwanza–Bukoba katika Ziwa Victoria.

Tafsiri

3. Katika Amri hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

Sura ya 415

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania;

Sura ya 212

"Kampuni" maana yake ni Kampuni ya Songoro Marine Transport Limited iliyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni;

"Shirika" maana yake ni Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania lililoanzishwa chini ya kifungu cha 4 cha Sheria;

"meli" maana yake ni meli zinazoendeshwa na Kampuni katika Ziwa Victoria.

SEHEMU YA PILI
NAULI NA MASHARTI YANAYOTUMIKA

Nauli zilizoidhinishwa

4. Kampuni inayoendesha meli-
(a) itatoza nauli kwa abiria isiyozidi viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Amri hii;
(b) itazingatia masharti ya utoaji huduma ya usafiri kwa njia ya maji yaliyoainishwa kwa mujibu wa Sheria ya Usafiri Majini. Sura ya 165

Masharti ya huduma

5. Wakati wa kutoa huduma, Kampuni itazingatia masharti yafuatayo:
(a) itaweka utaratibu maalum wa utambuzi wa abiria wenye mahitaji maalum kwa kuzingatia sheria zinazosimamia masuala ya walemavu na kuwasilisha utaratibu huo kwa Shirika ndani ya miezi mitatu tangu kuanza kutumika kwa Amri hii;
(b) itaweka utaratibu utakaowawezesha abiria wenye mahitaji maalum kusafiri bila vikwazo na kuwasilisha utaratibu huo kwa Shirika ndani ya miezi mitatu tangu kuanza kutumika kwa Amri hii;
(c) itawasiliana na uongozi wa Bandari ya Bukoba ili kuratibu ushushaji na upakiaji salama wa abiria bila kuathiri shughuli za watumiaji wengine wa Bandari;
(d) itabainisha katika tiketi gharama za upandaji na ushukaji wa abiria zinazotozwa na mamlaka nyinginezo, ikiwa zipo;
(e) itaimarisha mikakati ya kimasoko ili kuongeza idadi ya abiria; na
(f) itazingatia viwango vya usalama kama vilivyoainishwa katika Sheria ya Usafiri Majini na kanuni zake. Sura ya 165

**JEDWALI**

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 4(a))*

**NAULI KIKOMO ZILIZOIDHINISHWA KWA SAFARI YA MWANZA - BUKOBA**

| Daraja la Meli | Nauli ya Mtu Mzima (TZS) | Nauli ya Mtoto (TZS) | Nauli ya Mtu Mwenye Mahitaji Maalum (TZS) |
|---|---|---|---|
| Uchumi | 35,000 | 17,500 | 30,000 |
| Biashara | 50,000 | 22,500 | 40,000 |
| La Kwanza | 60,000 | 30,000 | 50,000 |

Dar es Salaam,
1st August, 2023

KAIMU ABDI MKEYENGE
*Mkurugenzi Mkuu*